

3. Madawa

Madawa ya cheti cha daktari na yasiyo na cheti

- daktari wako wa familia (GP) au daktari bingwa anaweza kukuwandikia dawa kwa kukupatia cheti.
- utahitaji kupeleka cheti hicho kwa duka la dawa.
- mfamasia atakupatia madawa hayo na kukufafanulia malipo, jinsi ya kutumia madawa hayo na kuangalia athari unazoweza kupata.
- Unaweza kununua baadhi ya vidonge, krimu na madawa ya maji bila ya cheti cha daktari. Hakuna ruzuku ya serikali kwa madawa yasio na cheti cha daktari.

Kulipia madawa yalio na cheti cha daktari

- Unapopeleka cheti hicho kwa duka la dawa, unapaswa kupeleka Kadi ya medicare, Kadi ya health care au Kadi ya Pensheni kwa maana hii itasaidia kufanya dawa iwe ya gharama ya chini.
- mpango wa faida ya madawa ya serikali kuu (PBS) hupunguza bei ya madawa yaliyo orodheshwa chini ya mpango huo.
- lazima daktari akundangie cheti cha dawa ili kufanya yastahiki mpango wa (PBS), hata hivyo sio madawa yote yanayoandikwa na daktari yako chini ya mpango wa PBS. Daktari wako akikuandikia madawa ambayo hayako katika orodha ya PBS itakubidi ulipie gharama yote
- kama una Kadi ya health care kiwango cha juu ambacho utalipia kila dawa ya PBS ni \$4.90 (kuanzia tarehe 1 Januari 2007)
- kama una kadi ya Huduma ya medicare cha juu zaidi ambacho utalipia kila dawaya kwa mpango wa PBS ni \$30.70 (kuanzia tarehe 1 Januari 2007)
- viwango hivi vya juu hurekebishwa kila tarehe 1 Januari ya kila mwaka.
- kama wewe au familia yako inahitaji madawa mengi kwa mwaka, muulize famasia wako kuhusu mpango mwingine unaoitwa 'Safety Net' ambao unaweza kukusaidia na gharama baada ya kufikia kiwango fulani cha pesa. Mfamasia wako anaweza kukusaidia kupata mpango huu.

Famasia wako anaweza kukuuliza kama unataka madawa ya yasio asili ambayo ni bei rahisi. Madawa mengi yanapatikana kwa aina zaidi ya moja na bei zinatofautiana baina ya aina hizo. Madawa yasiyo asili yana aina sawa ya viungo, nguvu ya aina moja, na vipimo sawa. Vile vile zimejaribiwa ili kuhakikisha kwamba zina athari ya aina moja kama madawa ya bei ghali.

Utumiaji wa madawa Utumiaji wa madawa

- Maelekezo ya kutumia dawa yataandikwa na kubandikwa kwenye dawa. Kama huelewi maelekezo hayo, muulize mfamasia akuelezee kwa maneno. Hakikisha kuwa :
 - hautumii madawa yaliyoandikiwa mtu mwingine
 - hautumii madawa yaliyopita wakati wake au yaliyoharibika
 - umeweka madawa mbali na watoto
 - unarudi kwa daktari wako ikiwa kuna athari zozote
 - haupatii mtu yeyote madawa uliyoandikiwa wewe hata jamaa au ndugu walio ng'ambo
 - umemfahamisha mfamasia au daktari wako ikiwa una matatizo wa kumeza madawa au unasahau kumeza madawa yako
 - umelewa jinsi ya kuhifadhi madawa yako – kwa mfano, baadhi
 - ya madawa yatahitajika kuwekwa kwa friji wakati madawa mengine hayastahili kuhifadhiwa kwenye friji
 - umewasiliana na mfamisia au daktari wako kabla ya kumeza au kutumia dawa
 - mpya yoyote ile ili kuhakikisha kwamba haziingiliani na madawa mengine unayotumia kwa wakati huo.

1. Adapted from Australia. The Victorian Foundation for Survivors of Torture Inc.[online] Aug 2001. [cited 26 April 2007] Available from: www.survivorsvc.org.au/pdfdocs/Healthy%20start/EnglishVersion.pdf

3. Madawa

Si kila wakati madawa yanaandikwa na daktari

- unaweza kuwa umengamua kwamba madaktari nchini Australia wanakuandikia madawa kwa njia tofauti na nchi uliotoka. Unaweza kuwa umepata madaktari nchini Australia wanasita kuidhinisha madawa, au kuonekana kutumia sindano kitofauti.
- madaktari wengi katika mfumo wa huduma ya afya ya Australia wanafahamu kwamba, kuwa na wasiwasi kunaweza kusababisha shida za afya ya kimwili. daktari wako anaweza kupendelea kuzungumza kuhusu shida zako, au mbinu za kutuliza hofu, badala ya kuidhinisha madawa.
- wakati daktari anapoamini kuwa mtindo wa maisha yako unaweza kudhuru au kukuza hali ya kiafya au kuzidisha magonjwa yako, Daktari anaweza kukushauri ubadilishe mtindo wa maisha yako kwa kufanya mazoezi, kula chakula bora au mambo ya burudani. Hii inaweza kuonekana ajabu; lakini, ushauri huu unatokana na utafiti wa afya bora.
- vile vile inawezekana kuwa unatumia madawa ya kienyeji au madawa ulionunua bila ya cheti cha daktari. Ni vizuri kumweleze daktari dawa zote unazotumia hata kama daktari hazitambui baadhi ya dawa hizo. Hii ni kwa sababu madawa ulioandikiwa na daktari yanaweza kuingiliana na kusababisha matatizo ya ki afya.

Kupata habari zaidi kuhusu madawa

- unaweza kupata maelezo zaidi juu ya athari za kawaida, madawa yanavyoingiliana, maonyo na habari zingine kuhusu madawa ya kuandikiwa na yale yasiyo ya kuandikiwa na daktari, pamoja na madawa yanayoendana (miti shamba/madawa ya kienyeji/vitamini/madini ya mwili) kwa kupigia simu ya Huduma ya Kitaifa ya madawa yanayoandikishwa (Nationa Prescribing Services - NPS) namba ya simu 1300 888 763 kati ya saa tatu asubuhi na saa kumi na mbili jioni, Jumatatu hadi Ijumaa. Tafadhali kumbuka kwamba wakalimani wa simu hawapatikani kupitia laini hii ya simu
- maelezo yaliyotafasiriwa katika lugha 16 kuhusu medicare, madawa ya PBS na jinsi ya kutumia madawa kwa usalama zinaweza kupatikana katika http://www.medicareaustralia.gov.au/yourhealth/our_services/choose_your_language.htm#d.

Karatasi hii ya kweli iko katika mfululizo wa 10. idadi kamili:

1. Mfumo wa afya nchini Queensland
2. Kumwona daktari
3. Madawa
4. Hospitali za Queensland
5. Vituo vya afya ya jamii
6. Huduma za meno
7. Afya ya pamoja
8. Kuishi na afya na kuzuia magonjwa
9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu
10. Wewe na mfumo wa huduma ya afya